# UHAKIKI WA MAIGIZO

Maigizo ni sanaa ambayo huwasilisha ana kwa ana tukio fulani kwa hadhira kwa kutumia usanii wa kiutendaji.

**Au**

Maigizo ni mpangilio wa maneno ambayo huambatana na utendaji wa wahusika. Wahusika huiga mambo mbalimbali yanayopatikana na jinsi yanavyotendeka katika jamii. Lugha ya wahusika wanaoigiza inaingiliana kwa kiasi kikubwa na lugha ya jamii husika.

## TANZU ZA MAIGIZO

Maigizo hujengwa kwa tanzu mbalimbali. Miongoni mwa tanzu hizoni:

**(a) Michezo ya jukwaani**

Ni mpangilio wa mazungumzo baina ya watu unaoambatana na utendaji wao. Mazungumzo hayo hujenga kisa chenye mgogoro au migogoro ya kijamii. Mgogoro huo unaweza kuwa baina ya ukale na usasa au uonevu dhidi ya haki.

**(b) Vichekesho**

Ni mpangilio wa maneno ulio na utendaji. Vichekesho huwa vina lengo la kufikisha ujumbe kwa njia ya kuchekesha au kufurahisha. Vichekesho huwa ni vifupi na havina uchambuzi wa ndani kuhusu kisa kinachooneshwa.

**(c) Majigambo:**

Haya ni maigizo ya kujitapa kwa mtu aliyefanya mambo ya maana au ya kishujaa katika maisha. Wahusika wa majigambo huwa ni watambaji ambao hutumia picha kali za mawazo na hisia na wanaonesha vitendo walivyovifanya ambavyo wanajivunia. Vitendo hivyo vinaweza kuwa kulima. Kuua Simba, kumdhuru adui na kadhalika.

**(d) Ngonjera:**

Ni mpangilio wa beti za mashairi ya kujibizana zinazoambatana na utendaji. Kila mhusika anatoa ubeti au beti zake huku akitenda vitendo mbalimbali vinavyoshabihiana na asemacho. Muundo wa ngonjera ni wa ushairi na huwa unatendeka.

## FANI NA MAUDHUI KATIKA MAIGIZO

Maigizo yana vpengele vikuu viwili kama ilivyo katika kazi zingine za fasihi. Vipengele hivyo ni fani na maudhui.

### i) Fani katika maigizo.

Katika maigizo, fani tunaangalia vipengele vifuatavyo:

**(a) Tendo au tukio**

Katika maigizo lazima pawepo na tendo au tukio kama kiini au chanzo cha utanzu huo. Hapa lazima pawe na vitendo vinavyotendwa. Tendo au tukio huwa ndiyo kishawishi cha fanani wa maigizo.

**(b) Wahusika:**

Katika maigizo huwa kuna wahusika wa aina kuu mbili ambao ni:

i) Watendaji (fanani)
ii) Watazamaji (hadhira)

**i) Watendaji**

Hawa ni wasanii ambao hutumia vipawa vyao kwa lengo la kuwasilisha dhana fulani kwa hadhira (wawasilishaji wa maigizo).Hawa hutumia mbinu mbalimbali kujenga kazi zao kuvutia hadhira. Katika igizo kuna mtendaji mkuu na watendaji wadogowadogo

- **Mtendaji mkuu,** ni yule anayejitokeza kila mara katika onesho fulani tangu mwanzo hadi mwisho. Huyu ndiye hubeba dhamira kuu ya igizo hilo.

- **Watendaji wadogowadogo,** hujitokeza hapa na pale katika onesho fulani ili kukamilisha onesho hilo. Hawa husaidia kujenga dhamira fulani katika igizo na vilevile husaidia katika kumjenga mtendaji mkuu. Lakini pia kuna watazamaji (hadhira) ambao wamekusanyika kwa makusudi ya kutazama igizo hilo. Watazamaji wanaweza kushiriki katika baadhi ya vitendo kama vile kuimba, kupiga makofi na kadhalika.

**ii) Watazamaji**

Hawa ni wale wanaoshiriki katika kuangalia tukio la kazi ya fasihi simulizi. Watazamaji huwa ni binadamu. Watazamaji katika fasihin simulizi huwa na kazi kuu mbili. Kwanza, kushiriki hata kwa kutazama kazi hiyo. Pili, kushiriki katika baadhi ya vitendo kama vile kuimba, kupiga makofi, kupiga vigelegele na kadhalika.

**(c) Mandhari (Uwanja wa kutendea)**

Maandhari ni mahali ambapo watendaji hutumia kuonesha onesho lao. Katika maigizo hapa huwa ni sehemu iliyotengwa kwa ajili ya igizo fulani. Mandhari yanaweza kuwa uwanjani, nyumbani, porini au jukwaani.

**(d) Muundo:**

Katika maigizo, muundo tunaangalia mpangilio wake. Yaani umbo lake lilivyogawika, kwenye sura au maonesho, mtiriko wa matukio na msuko. Matukio yanaweza kufuatana moja kwa moja au yakawa nenda rudi au changamano.

**(e) Mtindo:**

Maigizo hutumia mtindo wa dayolojia au majibizano baina ya wahusika waliopo katika jukwaa. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa mazungumzo hayo si maongezi au majibizano kwa ajili ya kujibizana tu. Mazungumzo hayo ni lazima yaendeleze tendo kuu katika maigizo.

**(f) Matumizi ya lugha**

Lugha ni nyenzo kuu ya maigizo. Dhamira na maudhui ya maigizo hayawezi kuwasilishwa na kuwafikia watazamaji bila kuwako lugha. Katika lugha, tunachunguza vipengele vifuatavyo:

**i) Matumizi ya methali**

Katika maigizo, methali hutumika:

- Kupitisha hekima
- Kujenga kejeli kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii.
- Kujenga mandhari ya kiutamaduni ya kuaminika kuhusu jamii.

**ii) Matumizi ya misemo na nahau.**

Katika maigizo lazima kuwepo na matumizi mbalimbali ya methali na misemo. Methali na misemo husaidia kuipamba kazi hiyo.

**iii) Tamathali za semi**

Tamathali za semi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana. Wakati mwingine tamathali za semi hutumiwa kwa ajili ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha. Tamathali za semi hizo ni kama zifuatazo:

➢ **Tamathali za mafumbo**

Tamathali za mafumbo ni kama zifuatazo:

- **Dhihaka:**
  Ni tamathali ya dharau na ina lengo la kumuweka mtu katika hali duni kupita kiasi lakini kwa lugha ya mafumbo.
  **Mfano:**
  Sophia alikuwa msichana msafi sana. Ndiyo maana kila mara alipaka mafuta yaliyonukia na kukaribisha nzi walioleta matatizo makubwa.

- **Tafsida**
  Hii ni tamathali ambayo hutumika katika kupunguza ukali wa wa maneno.
  **Mfano:**
  Kujisaidia – Kunya
  Kuaga dunia – Kufa.

- **Kejeli/ Shitizahi**
  Hii ni tamathali ambayo huleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo.
  **Mfano:**
  Mtu ni mchafu lakini anaambiwa sijamwona mtu msafi kama wewe.

- **Kijembe/kilinge**
  Huu ni usemi wa mzunguko. Ni usemi wa kimafumbo wa kumsema mtu kwa ubaya.

➢ **Tamathali za mlinganisho**
Tamathali za mlinganisho ni kama zifuatazo:

- **Tashibiha**
  Ni tamathali inayolinganisha vitu kwa kutumia maneno ya ulinganishi au viunganishi. Maneno hayo ni kama vile; sawa na, kama, mithili ya, mfano wa na kadhalika.

  **Mfano:**
  - John anakimbia <u>mithili ya</u> Swala
  - Pua ya Sara <u>ni kama</u> ya Tembo.

- **Sitiari**
  Ni tamathali inayolinganisha matendo, vitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti bila viunganishi.
  **Mfano:** - Suma <u>ni</u> Nyoka
  - Maisha <u>ni</u> moshi

- **Tashihisi**
  Ni tamathali ambayo vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo.
  **Mfano:**
  Mawimbi ya bahari yaliimba wimbo wa mahaba na kutufanya tupate usingizi.

➢ **Tamathali za msisitizo na nyinginezo**
Tamathali hizo ni kama zifuatazo:

- **Mubalagha**

Hii ni tamathali ambayo hutia chumvi au chuku uwezo wa viumbe, tabia zao na kuhusu sifa zao kwa madhumuni ya kuchekesha au kusisitiza.
**Mfano:** -
Tulikula mpaka tukatambalia migongo.

- **Metonimia/Taashira**

Ni tamathali ambayo jia la sehemu ya kitu kimoja au la ktu kidogo kinachotumiwa na kingine kikubwa hutumiwa kuwakilisha kitu kamili.

**Mfano:**
Jembe – Mkulima
Kalamu – Mwanafunzi.

- **Majazi**

Hii ni tamathali ambayo itajapo tu sehemu ya kitu papo hapo sehemu hiyo huashiria na kuwakilisha kitu hicho.

**Mfano:** Ajali ile iliua roho saba

- Roho – watu.

- **Taniaba**

Ni tamathali ambayo kwayo jina la mtu binafsi hutumiwa na watu wengine wenye tabia, mwenendo, hali au kazi sawa na ya mtu huyo.

**Mfano:**

Yesu wa kwanza Afrika Nkwame Nkurumah

Yesu – Mkombozi

- **Ritifaa**

Ni tamathali ambayo kwayo mtu huzungumza na kitu au mtu ambaye husikiliza katika fikra tu.

**Mfano:**

Ewe mwanangu lala vema katika tumbo la mama yako.

- **Tabaini**

Huu ni usemi unaosisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani.

**Mfano:**

- Amekuwa mrefu si mrefu, mfupi si mfupi ni wa kawaida tu.
-

- **Mbinu nyingine za kisanaa**

- **Takriri**

Ni mbinu ya kurudia rudia neno kwa lengo la kuweka msisitizo.

**Mfano:**

- Nilikwenda nilikwenda nilikwenda mpaka nikamkuta.
-

- **Mdokezo**

Ni maneno ambayo mwandishi au msemaji hukatiza maneno hayo au huyaacha bila kusema kinachoendelea.

**Mfano:**

Ningefika ila……

- **Tashtiti**

Ni mbinu ya kuuliza swali kwa jambo ambalo unalifahamu jibu lake.

**Mfano:**

Hivi ni kweli unakula?

- **Nidaa**

Ni msemo unaonesha kushangazwa kwa jambo fulani. Mseamo huu huambatana na alama ya mshangao.

**Mfano:**

Mungu wangu!

- **Mjalizo**

Ni mfuatano wa maneno yasiyokuwa na viungo vyovyote.

**Mfano:**

- Nilikaa, nikasubiri, nikachoka nikaondoka zangu.

- **Onomatopeia/Tanakali sauti**

Ni mbinu ya kuiga sauti mbalimbali katika kazi ya fasihi.

**Mfano:**

Alipodondoka alilia puu!
Viatu vyake vililia ko ko ko!

**(g) Taswira**

Ni picha zinazojitokeza katika kazi ya fasihi. Taswira hujitokeza baada ya matumizi mbalimbali ya semi na ishara. Matumizi mazuri ya taswira na ishara hutegemea ufundi wa mwandishi kuweza kuchota mambo mbalimbali yanayomzunguka yeye na jamii yake.

**Aina za taswira**

Taswira zinaweza kugawanyika katika aina mbalimbali. Aina hizo ni:

**(i) Taswira hisi**

Hii ni taswira ambayo hushughulika na hisi ya ndani. Taswira hii huweza kumfanya msomaji au msikilizaji awe na wasiwasi, aone woga, apandwe na hasira au asikie kinyaa. Taswira hii huwa na nguvu kubwa ya kuganda akilini.

**Mfano:**

Akaniambia, “siwezi kula chakula hicho rojorojo mfano wa kohozi lenye sumu”.

**(ii) Taswira ya mawazo/ Kufikirika**

Ni taswira inayotokana na mawazo. Mawazo hayo ni yale yanayohusu mambo yasiyoweza kuthibitika. Mambo hayo ni kama vile:

- Kifo
- Njaa
- Uchungu
- Raha na kadhalika.
-

**Mfano:**

Kifo! Kifo! Umetufanya nini sasa, mpaka unaamua kutuchukulia ndugu yetu?

**(iii) Taswira zionekanazo**

Hii ni tawira ambayo hujengwa kwa kutumia vielezo tunavyovijua au vile vinavofahamika katika katika maisha ya kila siku.

**Mfano:**

"Haikupita dakika mijusi miwili ilipita mbele yetu. Midomo yao ilikuwa mekundu, ghafla walikutana na nyoka aliyeonekana mnene tumboni. Hapana shaka alikuwa amekula mnyama".

**(h) Ucheshi**

Ni mbinu ya kifani ambayo wasanii hutumia katika kazi zao za kifasihi ili kuchekesha hadhira zao au kuzifanya hadhira zao zitabasamu. Mbinu hii ya ucheshi hutumiwa na wasanii mbalimbali kwa makusudi yafuatayo:

- Kuwafurahisha wasomaji wa kazi zao
- Kuondoa uchovu kwa hadhira zao.
- Kukejeli katika kazi zao.

**(i) Upeo/ Kilele**

Upeo au kilele katika maigizo ni sehemu inayokidhi haja ya hadhira inayopokea kazi hiyo. Katika sehemu hii watazamaji hupata majibu muhimu ambayo igizo au onesho huwa imeyachelewesha kwa kutumia mbinu kadhaa kama vile taharuki au mbinu rejeshi.

Sehemu hii mara nyingi husisimua watazamaji katika hali ya juu sana. Katika maigizo, watendaji hujenga migogoro ambayo hujitokeza na kukua kama jinsi ambavyo kazi hizo zikuavyo.

**ii) Maudhui katika maigizo**

Uhakiki wa maudhui katika maigizo huzingati vipengele vifuatavyo:

**(a) Dhamira**

Hili ni wazo kuu au mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika onesho fulani. Hapa kuna dhamira kuu na dhamira ndogondogo.

**(b) Ujumbe na maadili**

Katika maigizo ujumbe ni mafunzo mbalimbali tunayoyapata baada ya kuona na kusikia igizo au onesho fulani. Ujumbe huambatana na maadili mbalimbali.

**(c) Migogoro**

Migogoro ni mivutano mbalimbali inayojitokeza katika maigizo. Migogoro inaweza kuwa kati ya mtu na mtu familia na familia, tabaka na tabaka na kadhalika. Migogoro inaweza kuwa ya:

- Kiuchumi
- Kisiasa
- Kiutamaduni na kadhalika.

**(d) Falsafa**

Ni muelekeo wa imani ya msanii. Falsafa ya kazi ya sanaa inatakiwa ichambuliwe kwa kuzingatia jinsi kazi hiyo inavyoutazama ulimwengu unaohusu kuhusu ukweli juu ya mambo mbalimbali.

*Kwa kumalizia tunaweza kusema kuwa kuna wakati wa kuchambua maudhui ya igizo fulani. Maswali mbalimbali yanaibuka:

- Je, msanii anatueleza nini?
- Msanii kamtungia mtu wa tabaka gani?
- Anamtukuza nani?
- Msanii anatutaka tuchukue hatua gani katika utatuzi wa matatizo anayoyashughulikia katika kazi yake.
- Je, ni api masuala makuu katika onesho fulani?